




Joyce's Story

Joyce was defiled by a neighbor who was a watchman. Joyce told her sister about the defilement, who told her friends in the Justice Club at school. The Club members helped Joyce gain enough confidence to tell the Club patron/teacher, and together they informed the patron/teacher of the defilement. As a group, in solidarity, the Justice Club leaders accompanied Joyce and the Club patron to the police station to report the defilement. The police investigated the case and perpetrator was arrested and the matter is proceeding in court. *Note: Joyce is not her real name.*


Forms of Sexual Violence

Sexual violence takes many forms, including **rape, sexual assault, defilement, and incest** (any kind of sexual interaction between people who are related to each other). Sexual violence can be: (1) **unwanted touching** in a sexual way, such as kissing, grabbing, or fondling; (2) **unwanted attempted intercourse**: this occurs when someone attempts to engage in sexual intercourse with someone who doesn't want to; (3), **pressured intercourse** in which someone is pressured or threatened in some other way to have sexual intercourse against his or her will or; (4) **physically forced intercourse** in which someone is physically forced to have sexual intercourse against his or her will.



Age of Consent

All of these violent acts are unwanted, and **non-consensual**. This means that the person who is being violated did not agree to be touched sexually or engage in any kind of sexual act. In Kenya, **the age of consent is 18 years old**. This means that a person who is younger than 18 years of age cannot legally consent to a sexual act. Any time a person of any age has sex with a minor, it is called defilement and it is a criminal offense, no matter how the child responded or acted. Only adults can consent to sex. When you're an adult, giving someone your consent to engage in any kind of sexual activity means that you are telling them that you want to do this with them. If you feel uncomfortable or unsafe at any time during a sexual encounter, you have the right to take back your consent. Even if you said yes at first, you can ask to stop at any time. When you're under 18, you cannot give consent at all.



Coercion and Manipulation

Perpetrators will sometimes coerce or manipulate a child into thinking that they want to have sex with them. In our societies, children are taught to obey adults/elders and do as they are told. Unfortunately, sometimes adults/elders will use this power to take advantage of children and control them. This allows some adults/elders to coerce or manipulate children into uncomfortable or dangerous situations, such as sexual assault or rape. **Children are not able to give consent, because they cannot completely understand the emotional or physical negative effects of sexual assault.** If someone tries to force a child to have sex, but is unsuccessful, this is an attempted rape. All rapes, including attempted rapes, are **crimes** and should be reported to the police.

COMMUNITY CORNER

This week, we asked the Justice Club leaders: how would you react if someone you trusted tried to convince you to have sex with them, knowing sex with an adult is wrong and illegal? What would you do in this situation?



Magenta Piano from Kakamega:

"Say no! and report the perpetrator at the near by police station."

Calm Waterfall from Mombasa:

"If someone I trusted tried to convince me to have sex with him, my first response NO and NO. I will insist to say NO because my right and protection and MUST be respected. Secondly, report the matter to the nearest Local Rape Rescue Partner or to the nearest police station. I will make sure that the matter is investigated by police officer and action is taken. I will stand firm and make sure that the police officer take the person is taken to court because having sex with [a child] is wrong and illegal."



Adorable Lion from Nairobi:

"I'll report it to a police officer or the nearest police station, or call the child helpline and tell it to a trusted justice club leader."

To Report a Defilement

To download the free **160 Girls defilement reporting app**: scan the QR code (right) by pointing your phone's camera at the code. The app's web page will appear with an option to download the app. You can also search "160 Girls app" in your phone's app store or submit a "help request" on 160girls.org.



You can also connect with your local rape rescue partners:

KARE (Kakamega)

Tel: 0724721671/0721782381

E-mail: kare.org@gmail.com

Website: karemp.org

GVRC (Nairobi)

Tel: 0713513141/0719638006

E-mail: gvrc@nwch.co.ke

Website: gvrc.or.ke

ICRH (Mombasa)

Tel: 0722208652/0734466466

E-mail: info@icrhk.org

Website: icrhk.org

They can offer support, and help you report the defilement to the police. You can also report to the police on your own, or talk to a trusted friend or relative.





Kisa cha Joyce


Joyce alinajisiwa na jirani ambaye pia ni mlindalango. Joyce alimwamweleza dadake kuhusu unajisi huo, ambaye pia aliwaeleza marafiki zake katika Justice Club pale shuleni. Wanachama wa Justice Club walimsaidia Joyce kupata ukakamavu wa kutosha kumwambia mlezi wao/mwalimu. Kwa pamoja walimweleza mlezi/mwalimu wao kuhusu kisa hiki. Kama kikundi na kwa ushirikiano viongozi wa Justice Club waliandamana na Joyce pamoja na mlezi wao hadi kwenye kituo cha polisi ambako waliripoti kisa hicho cha kunajisiwa kwa Joyce. Polisi walichunguza kisa hicho na kumkata mnajisi huyo. Kesi hiyo bado inaendelea kuskizwa kortini.

Aina za Dhulma za Kimapenzi

Dhulma za kimapenzi ni za aina mbalimbali ikiwemo; ubakaji, mashambulio ya kingono; unajisi, na uchumba (incest – aina yoyote ya uhusiano wa kingono kati ya watu wa familia moja). Dhulma za kimapenzi zinawezakuwa: (1) kuguswa kusikofaa au kukubalika kama vile busu, kushikwa sehemu isiyofaa, au kupapaswa; (2) kuingiliwa au mtu kujaribu kukuingilia kimwili bila idhini/ruhusa yako: hii hutokea pale mtu anapojaribu kufanya ngono na mtu asiyetaka kufanya kitendo hicho; (3) ngono ya kulazimishwa kwa njia moja au nyingine au; (4) ngono ya kimabavu ambapo mtu hulazimishwa kufanya ngono bila kutaka au kinyume na msimamo wake.

Umri unaokubalika kufanya ngono

Matendo haya yote ya kimabavu hayakubaliki na wala mtendwa huwa hajayakubali. Hii inamaana kwamba yule aliyedhulumiwa hakukubali kuguswa kwa njia isiyofaa au kutenda kitendo chochote cha ngono. Nchini Kenya, mtu anaweza kukubali kufanya ngono ikiwa amefikisha umri wa miaka kumi na minane (18 years). Hii inamaanisha kuwa mtu yeyote aliye na umri chini ya miaka kumi na minane (18 years) hawezi kukubaliwa kufanya ngono nawe – kisheria. Wakati wowote mtu anapofanya ngono na mtoto mwenye umri chini ya miaka 18, hicho kitendo huchukuliwa kuwa unajisi na ni kosa la jinai. Hii haijalishi alivyotenda mtoto huyo. Ni watu wazima pekee (wenye umri wa zaidi ya miaka 18) wanaoweza kukubali kufanya ngono – kisheria. Ikiwa wewe ni mtu mzima bila shaka unapomkubalia mtu kufanya nawe ngono inamaanisha kwamba unajua kile unachokifanya na kwamba umemkubalia kufanya nawe kitendo hicho. Hata hivyo, ikiwa utahisi kutokuwa salama au kupendelea kitendo hicho, una haki ya kukataa kuendelea na kitendo hicho kwa wakati wowote, hata kama ulikuwa umekubali kufanya kitenda hicho hapo mbeleni. Ikiwa una umri wa chini ya miaka 18 huwezi kumkubalia mtu kufanya kitendo cha ngono nawe hata kidogo.





Kulazimishwa na Kuhadaiwa

Wakati mwingine wanajisi huwalazimisha au kuwahadaa watoto ili waamini kuwa ndio waliotaka kufanya mapenzi nao. Katika jamii yetu watoto wanafunzwa kutii watu wazima au wazee. Kwa bahati mbaya wakati mwingine watu wazima au wazee hawa hutumia mafunzo haya kuwahadaa watoto kufanya nao mapenzi. Hali hii huwafanya watu wazima au wazee hao kuwalazimisha au kuwahadaa watoto na kuwadhulumu kimapenzi au kuwabaka. Watoto hawawezi kutoa idhini ya kufanya ngono kwani hawaelewi kikamilifu madhara yake ya kihisia au kimwili – hasa dhulma za kimapenzi. Ikiwa mtu atajaribu kumlazimisha mtoto kufanya mapenzi naye lakini asifaulu, hiyo itakuwa sawa na ubakaji. Aina zote za ubakaji ni makosa ja jinai (crime) na zinafaa kuripotiwa kwa polisi.

Pembe ya Kijamii

Wiki hii tuliwauliza viongozi wa Justice Clubs: Je, utafanyaje ikiwa mtu unayemwamini atajaribu kukushawishi kufanya naye mapenzi hasa ukifahamu kuwa kufanya ngono na watu wazima ni vibaya na hatia? Utafanyaje ukijipata katika hali kama hii?



Alisema Magenta Piano kutoka Kakamega:

"Sema la! na umshataki mhalifu katika kituo cha polisi kilicho karibu."

Alisema Calm Waterfall kutoka Mombasa:

"Iwapo mtu ninayemwamini ananishawishi nifanye mapenzi au ngono naye, jambo la kwanza nitasema ni La! Hapana! Nitaendelea kusema LA kwa sababu ni haki yangu na LAZIMA iheshimiwe. Pili, nitaripoti kisa hicho kwa shirika la kuwaokoa watoto dhidi ya ubakaji ama kituo cha polisi. Nita hakikisha kisa hicho kimechunguzwa na polisi na hatua kuchukuliwa. Nitasimama imara na nihakikishe polisi wamemshtaki mhusika mahakamani kwasababu kufanya ngono na {mtoto} ni vibaya na ni hatia."



Alisema Adorable Lion kutoka Nairobi:

"Nita ripoti kisa kwa afisa wa polisi ama kituo cha polisi, ama nipige simu kwa laini ya msaada wa watoto na na nimweleze kiongozi wa kilabu cha haki (justice club) ninayemwanini."

Ili Kuripoti Unajisi:

Pakua (Download) app ya 160 Girls inayohusu kuripoti visa vya unajisi (160 Girls defilement reporting app): skana (scan) msimbo wa QR (QR code) - ulio upande wa kulia kwa kuumulika kwa kamera ya simu yako. Wavuti (website) ya app hiyo itafunguka na kuashiria 'Download'. Vilevile unaweza kuitafuta app hiyo kwenye app store yako au kutuma ombi kwa 160girls.org



Unaweza pia kushirikiana na wadau wa unajisi waliokaribu nawe:

KARE (Kakamega)

Tel: 0724721671/0721782381

E-mail: kare.org@gmail.com

Website: karemp.org

GVRC (Nairobi)

Tel: 0713513141/0719638006

E-mail: gvrc@nwch.co.ke

Website: gvrc.or.ke

ICRH (Mombasa)

Tel: 0722208652/0734466466

E-mail: info@icrhk.org

Website: icrhk.org

Hawa wanaweza kukupa msaada pamoja na kukusaidia kuripoti unajisi huo kwa polisi. Vilevile, unaweza kuripoti kwa polisi mwenyewe au kumweleza rafiki au jamaa yako.

